

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**



**TAARIFA YA IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI.**

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**

## **YAH: - IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI.**

### **1.0 UTANGULIZI.**

Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ilianzishwa rasmi kwa Tangazo la serikali Na.446/2013(GN No.446 of 2013) tarehe 1.7.2013.

Idara ya Mipango,Takwimu na ufuatiliaji ni moja kati ya Idara zake za kuwezesha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi ili kupunguza na hatimaye kuondoa kero za wananchi.

### **2.0 WATUMISHI WALIOPO HADI SASA.**

Idara hii kwa sasa ina watumishi wanne kama ifuatavyo:-

- a) ALLI SAID SHEMNDOLWA-MKUU WA IDARA
- b) DANIEL RICHARD TESHA-MTAKWIMU
- c) FESTO DAVID MATEWA-MTAKWIMU
- d) BENJAMIN DAVID NKWERA-MCHUMI

### **3.0 MAJUKUMU YA IDARA**

Majukumu ya Idara ya mipango ,takwimu na ufuatiliaji ni kama ifuatavyo:-

- a) Kukusanya takwimu za kiuchumi na kijamii
- b) Kuchakata na kutafsiri takwimu za kiuchumi na kijamii
- c) Kuunganisha matokeo ya mchakato wa takwimu za kiuchumi na kijamii
- d) Kuibua miradi ya maendeleo kwa kutumia mbinu shirikishi jamii ya fursa na vikwazo iliyoboroshwa.
- e) Kutathmini matokeo ya uibuaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia mbinu shirikishi jamii ya fursa na vikwazo iliyoboreshwa.

- f) Kupanga mpango wa maendeleo wenye miradi iliyoibuliwa kwa kuzingatia mbinu shirikishi jamii ya fursa na vikwazo iliyoboreshwa.
- g) Uratibu na uthibiti wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa kufanya mapitio kila wakati.
- h) Uhifadhi wa takwimu za kiuchumi na kijamii.
- i) Kuratibu na kusimamia mchakato wa maandalizi ya Bajeti na mpango wa maendeleo wa mwaka.
- j) Kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo za robo mwaka ,nusu mwaka na mwaka mzima.
- k) Kuratibu na kusimamia masuala ya jinsia katika shughuli zote za maendeleo.

#### **4.0 SHUGHULI MUHIMU ZILIZO RATIBIWA NA ZILIZO TEKELEZWA TOKA HALMASHURI YA WILAYA YA MKALAMA ILIPOANZISHWA.**

1. Ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya Halmashauri.
2. Ujenzi wa ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.
3. Ujenzi wa shule za sekondari 19
4. Uanzishaji wa kidato cha Tano katika shule ya sekondari Iguguno.
5. Upimaji wa viwanja 531 katika mji wa Nduguti.
6. Uchongaji wa barabara mpya za mji wa nduguti.
7. Uchimbaji wa visima 47 kwa maeneo yasiyoyapata huduma huko vijijini.
8. Kuimarisha kituo cha afya kinyambuli kiweze kutoa huduma ya upasuaji.

#### **5.0 TAMATI**

**Kuna changamoto nyingi hususani ni kwa kuzingatia ukweli kuwa hii ni wilaya ukweli kuwa hii ni wilaya mpya na changa.**

Mikakati ya kutatua na kuondoa kero za wananchi ni hii ifuatayo:-

- a) Kuanzisha Hospitali Teule ya wilaya ya Iambi.

- b) Kujenga Hospitali ya wilaya katika mji wa Nduguti kwa kushirikisha jamii na wadau mbalimbali
- c) Kuanzisha kidato cha tano na sita katika shule ya Sekondari Gumanga. Hata hivyo yote yaliyopangwa na mengine mengi yatawezekana kutekelezwa kwa kudumisha Amani na upendo na ushirikishwaji na jamii katika shughuli za Maendeleo.

NAWASILISHA

.....

ALLI SHEMNDOLWA

KNY MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**MKALAMA**